

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

06

URAI NA MAADILI

Muda: Saa 1:30

Mwaka 2020

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenye jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A ina alama **ishirini na sita (26)** na sehemu B ina alama **ishirini na nne (24)**

SEHEMU A (Alama 26)

1. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku.
 - (i) Ngoma ya asili ya watu wa mkoa wa Ruvuma huitwa
A. mganda B. mdundiko C. mdumange D. sindimba []
 - (ii) Moja kati ya mambo yanayovutia watalii katika nchi ya Tanzania ni
A. barabara na ufugaji wa kuku
B. bustani na za maua na mvua
C. milima na Hifadhi za Taifa
D. viwanja vya michezo na mabwawa ya samaki []
 - (iii) Zipi kati ya nchi zifuatazo sio wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?
A. Tanzania na Uganda C. Rwanda na Burundi
B. Kenya na Uganda D. Zambia na Zimbabwe []
 - (iv) Shughuli gani ya asili inayofanywa na jamii ya watu waishio karibu na bahari au maziwa?
A. Ufugaji wa samaki C. Uvuvi wa samaki
B. Uchimbaji wa mabwawa D. Kilimo cha mpunga []
 - (v) Zamani viongozi wa makabila walipatikana kwanjia gani?
A. Kurithishwa B. Uchaguzi C. Uteuzi D. Kupendekeza []

2. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuoanisha maana ya maneno katika **Fungu A** na maneno sahihi katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

Fungu A	Herufi	Fungu B
(i) Hutoa taarifa kwa njia ya sauti tu	[]	A. Gazeti B. Maabara C. Maktaba
(ii) Hutoa taarifa kwa njia ya picha na maneno tu	[]	D. Masimulizi E. Radio F. Runinga
(iii) Hutoa taarifa kwa njia ya picha, maneno na sauti	[]	
(iv) Hutoa taarifa kwa njia ya Mazungumzo	[]	

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.


- (i) Watoto walitoa ushahidi wa kweli juu ya wizi uliofanywa na wenzao. Kitendo walichofanya watoto kinaonesha nini? _____
(uaminifu, upendo, usaliti)
- (ii) Mtu ambaye ana umri wa chini ya miaka 18 huitwa _____
(kijana, mtoto, mtu mzima)
- (iii) Chombo kipi kisicho cha kiserikali kinachohusika na haki za binadamu katika Tanzania? _____ (TAMWA, Bunge, Polisi)
- (iv) Mtu kutoaminika kwa wengine yaweza kuwa ni matokeo ya mtu huyo _____
(kutokuwa muwazi, kuwa mnyenyekevu, kuwa mchapakazi)

SEHEMU B (Alama 24)

4. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuonesha matendo yanayoonesha **kujipenda** au **kuwapenda wengine** kwa kuweka alama ya (✓) kwenye sehemu inayohusika. Namba (i) imejazwa **kama mfano**.

Kitendo	Kujipenda	Kuwapenda wengine
(i) Subira anawaoggesha wadogo zake kila siku		✓
(ii) Jumanne anafua sare zake za shule na kuzipiga pasi kila siku.		
(iii) Juma alimshukuru Roda kwa kutoa msaada kwa mama yake aliyekuwa mgonjwa		
(iv) Amina anapiga mswaki na kuoga kila siku		
(v) Mwanafunzi alitoa pole kwa mwenzie aliyepata matatizo		

5. Chunguza kwa makini picha ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.



Maswali:

- (a) Ni rasilimali gani inaharibiwa katika picha hii? _____
 - (b) Ni njia gani wanatumia kuharibu rasilimali iliopo kwenye picha hii? _____
 - (c) Ni kifaa gani wanatumia kuharibu rasilimali hii? _____
 - (d) Uharibifu wa rasilimali hii husababisha nini _____
6. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

Shule ni mahali ambapo ufundishaji na ujifunzaji hufanyika. Matendo ya ufundishaji na ujifunzaji ni kama vile kuhesabu, kusoma, kuandika, kuchora, kucheza na kuonesha tabia njema.

Tunakwenda shuleni mapema asubuhi na kufanya usafi kwenye mazingira ya shule. Kengele ikigongwa, tunasimama kwenye mstari na kusikiliza matangazo mbalimbali. Baada ya hapo tunaingia tayari kuanza masomo saa mbili kamili asubuhi.

Kila Ijumaa ni siku ya michezo. Tunamaliza masomo saa 6 kamili. Tunakwenda viwanjani kushiriki katika michezo. Tunacheza michezo ya aina tofauti kama vile mpira wa miguu, mpira wa mikono, kuteleza, ukuti, kukimbia na kubembea.

Maswali:

- (a) Taja shughuli kuu mbili zinazofanyika shuleni.
- (b) Ni kwanini wanafunzi husimama kwenye mistari kila kengele inapogongwa? _____
- (c) Ni muda gani vipindi huanza? _____
- (d) Ni siku gani masomo huisha saa 6 kamili? _____